

Aidha, nitumie fursa hii kuwaasa na kuwakumbusha wapiga kura umuhimu wa kutunza kadi zao. Wapiga Kura walioandikishwa kwenye daftari la Kudumu la Wapiga Kura wasiruhusu mtu yeyote kuchukua kadi zao za mpiga kura kwa lengo lolote na kwa namna yoyote ile. Kwa mujibu wa kifungu cha 90(2) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, ni kosa la jinai kwa mtu yeyote kuchukua kadi ya mpiga kura iliyotolewa kwa mtu mwingine. Zipo taarifa zinazofanyiwa uchunguzi za watu wanaopitapita wakikusanya kadi kwa kutumia ushawishi, ulaghai na udanganyifu kuwa watatoa mikopo baada ya kupokea kadi kutoka kwa wapiga kura.

Natoa tahadhari kwa wananchi kuepuka kutenda kosa la kuchukua kadi ya mpiga kura yeyote kinyume cha Sheria. Aidha, Wapiga kura wasikubali kudanganywa, wala kulaghaiwa au kushawishiwa kutoa kadi zao za mpiga kura kwa mtu yeyote. Kila mpiga kura aone umuhimu wa kutunza kadi yake vizuri katika kipindi hiki tunapoelekea kwenye Uchaguzi Mkuu wa tarehe 28/10/2020.



**Jaji (R) (Mst) Semistocles S. Kaijage**

**MWENYEKITI**

**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**